JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI KAZIMA,

S. L. P 369,

TABORA.

22/03/2022.

SIMU: MKUU WA SHULE 0629 443 071
0788 400 218

MKUU MSAIDIZI 0766 004 042

KUMB: NA _____

MZAZI/ MLEZI/ WA _____

S. L. P _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAZIMA - TABORA KIDATO CHA TANO 2022.

- Ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao _____amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO (BWENI) katika shule hii kwa mwaka huu wa masomo 2022/2023. Hivyo nachukua fursa hii kukupongeza saana wewe na mwanao.
- Shule hii (Kazima Sekondari) ipo Mjini Tabora. Mita 200 Kusini Magharibi ya kituo cha Reli (Tabora Railway Station) na kilomita 1.5 Mashariki ya kituo kikuu cha Mabasi Tabora Mjini – karibu kabisa na ORION TABORA HOTEL. Hivyo unaweza kusafiri toka uliko na kufika shuleni kwa Barabara (Mabasi) ama kwa Reli (Gari Moshi la abiria)
- Anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …… kwa ajili ya usajili tayari kuanza masomo kwa muhula wa kwanza.
- Mara upatapo barua hii na kuisoma kwa makini, tafadhali unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji yote stahili (yaliyoorodheshwa) ili kumwezesha afike shuleni mapema bila kupoteza muda wa masomo.

1. Mambo muhimu ya kuzingatia.

Sare ya shule

(a) Wasichana wote sketi rangi ya damu ya mzee (kitambaa cha suti) ndefu hadi kwenye vifundo vya mguu, marinda yenye ukubwa sentimita 5 kuzunguka sketi, shati jeupe mikono mifupi lisilobana na liwe refu

(b) Wasichana waislamu, sketi ya damu ya mzee (kitambaa cha suti) ndefu hadi kwenye fundo la mguu, marinda makubwa mawili nyuma na mbele, nusu kanzu nyeupe (tetroni) ndefu kuvuka kiuno, juba jeupe (tetroni) refu kuvuka kiuno

(c) Wavulana : suruali rangi ya damu ya mzee(kitambaa cha suti), yenye marinda mawili isiyobana upana wa chini uwe inchi 18 – 24 shati jeupe mikono mifupi lisilobana na lisiwe fupi

(d) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

(e) Sare ya mchezo / mazoezi: ni tracksuit rangi ya damu ya mzee na raba.

(f) Soksi za darasani ni rangi nyepe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana

(g) Mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana

(h) Sweta rangi ya damu ya mzee

(i) Nguo za kushindia ni T – shirt (2) za damu ya mzee yenye kola nyeupe na ufito wa damu ya mzee, suruali ya damu ya mzee (wavulana), gauni la damu ya mzee lanye kola nyeusi (wasichana) juba jeupe (wasichana wa kiislamu)

(j) Tai ya rangi ya damu ya mzee .

(k) Blanketi ya rangi ya kijivu na chandarua rangi Nyeupe.
(l) Sketi ya michezo damu ya mzee fupi yenye kufungwa kwa kamba.
(m) Tisheti (fulana) ya damu ya mzee isiyo na kola kwa ajili ya michezo.

1.1 Ada na michango ya shule

a) Ada

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula. Fedha hizo zilipwe kwenye account ya shule namba 51001100068 jina la account ni **Kazima Sekondary School Revenue Collection** (NMB)

Hakikisha linnandikwa jina la mwanafunzi kwenye sehemu ya muwekaji kwenye risiti ya benki' Benki Pay Slip. Mwanafunzi aje na Bank Pay Slip halisi (original BPS) ambayo inaonyesha michango aliyolipa.

b) Michango ya shule

i. Ukarabati wa samani za shule Tshs. 15,000/=
ii. Kitambulisho na picha Tshs. 6,000/=
iii. Taaluma Tshs.20,000/=
iv. Posho ya wapishi Tshs 30,000/=
v. Ulinzi Tshs. 15000
vi. Nembo ya shule Tshs. 2,000/= kwa nguo moja
vii. Huduma ya kwanza Tshs. 10,000/=
viii. Mtihani wa utimilifu kanda ya magharibi Tshs 20,000/=

Jumla ya michango yote ni 118, 400/=

- Shilingi 90,000/= zilipwe benki kweye akaunti ya shule 51001100086 **Kazima Sekondary School Project Account NMB.** Pia mwanafunzi aje na Bank Pay Slip inayoonyesha kiasi alicholipa.

- Shilingi 28,000/= (Mitihani ya utimilifu ya kanda, kitambulisho na nembo) ziletwe mkononi.

NB: Kwa mwanafunzi asiyekuwa na Bima ya Afya, aje na Tshs 50,400/= kwa ajili ya BIMA YA AFYA (NHIF)

c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**.

i) Ream 1 za karatasi kwa muhula. (ream 2 kwa mwaka)
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi anayosoma
iii) Dissecting kit kwa mwanafunzi wanaosoma somo la biology

iv) Scientific Calculators kwa wanaosoma tahasusi za PCM, PCB, EGM, HGE na ECA

v) Godoro la futi $2\frac{1}{2}$ upana

vi) Mashuka jozi 2 rangi ya pinki, mto, chandarua pembe nne futi nne kwa sita

vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,kijiko na kikombe)

viii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko, dumu la lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa.

ix) Vifaa vya usafi, jembe lenye mpini, kwanja 1, panga 1, fagio la ndani (soft broom), fagio la maji (squeezer), fagio la nje na mundu 1.

2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA

(i) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.

(ii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iii) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla

(iv) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule

(v) Kusuka nywele. Wamafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(vi) Kufuga ndevu.

(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(viii) Uvutaji sigara

(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuo au kuolewa

(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba.

(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria ya nchi.

(xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(xv) Kudharau bendera ya Taifa.

(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.

(xvii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

3. Mwanafunzi ataje ndugu au jamaa wanne wa karibu ambao shule itawatambua na kuwasiliana nao mara anapohitajika. Picha (passport size) za ndugu hao aje nazo mwanafunzi wakati wa kuripoti shule

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KAZIMA SEKONDARI



ELIZABETH N. MASANJA

MKUU WA SHULE



SHULE YA SEKONDARI YA KAZIMA

A. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI……..
2. TAREHE YA KUZALIWA……
3. MZAZI / MLEZI ……
4. UHUSIANO NA MLEZI ……..
5. MAHALI UNAPOISHI MZAZI / MLEZI, MKOA…… WILAYA …… MTAA/KIJIJI…….
6. MAWASILIANO YA MZAZI / MLEZI…….
7. KABILA …….
8. KAZI YA MZAZI/ MLEZI ……
9. WAZAZI WAKO HAI AU WAMEFARIKI WEKA ALAMA YA (√)
    - BABA (AMEFARIKI) ( ) BABA YUPO HAI ( )
    - MAMA(AMEFARIKI) ( ) MAMA YUPO HAI ( )
10. NDUGU WENGINE WA KARIBU NA MZAZI / MLEZI AMBAO WANAWEZA KUTUMIKA KAMA WALEZI WA WANAFUNZI KAMA MZAZI / MLEZI HUSIKA HAYUPO
    a) …… MAHALI …….
    b) …… MAHALI…….
    c) …… MAHALI…….
    d) ……. MAHALI……

B. MAKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (jina la mwanafunzi) …….. nimesoma na kuelewa sheria, kanuni za taratibu za shule ya bweni, niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapo kuwa shule adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

…… .. …….

Saini ya Mwanafunzi Saini ya Mkuu wa shule

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY

KAZIMA SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 329

TABORA

……

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

This form must be completed by a government medical officer

Student's full name……

Present age…….

Blood test …….

School examination ……..

T.B test……

Asthma ……

Eye disorder ……

Nose disorder ……..

Ear disorder …….

Skin disease ……\

Anaemia ……

Chest …….

Operations …….

Serious accidents …….....

Any other infections disease ……..

Pregnancy …….

Additional information e.g. physical defects or impairment, chronic or family diseases

etc……

…….

I certify that I have personally examined Mr./miss ……and found him/her fit unit to purpose studies

Signature…….

Designation…….

(Official rubber stamps)……